# Zab 15 - Utuonyeshe njia ya uzima

**Siku ya Mungu ya tatu ya Paska, Mwaka A**

Eugène AMPIRE Bisimwa







1. Ee Mungu, unilinde, kwa maana nakukimbilia.
   Namwambia Bwana: "Wewe ni Bwana wangu".
   Bwana ndiwe urisi wangu na kikombe changu:
   Ndiwe unayenilindia mali yangu.

2. Namtukuza Bwana aliyenipa shauri,
   Kweli moyo wangu wanifundisha hata usiku.
   Namweka Bwana daima / mbele ya macho yangu.
   Sitatikisika kwa maana yupo kuumeni kwangu.

3. Kwa hiyo moyo wangu waona furaha,
   Nayo roho yangu yatoa shangwe,
   Hata mwili wangu / utapumzika salama.
   Kwani hutaiacha roho yangu kuzimuni, Wala hutamkubali mwamini wako aingie shimoni.

4. Kwangu hakuna heri, ila katika Wewe!
   Unanionyesha njia ya uzima,
   Wingi wa furaha / mbele ya uso wako,
   Anasa za milele kuumeni kwako